Mwongozo wa Kiongozi
Maombi ya Nadhiri
Kushirikishana na kusimuliana uzoefu wa maisha yetu ya imani
Kifungu cha Biblia 1 Samwel 1:7-20
Maombi ya Hana ya Nadhiri

MKUSANYIKO

Kiongozi wa mkutano awakaribishe watu kadri wanavyoingia mmoja mmoja na kuketi katika viti.
Baada ya watu wote kuwa wamekaa katika viti: Kiongozi awaombe wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha asome kwa sauti ya kusikia kifungu hiki cha Biblia

KIFUNGU CHA BIBLIA

Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. (Wafilipi 4: 6-7).

Kiongozi awaombe washiriki wa mkutano wote wavute pumzi ndefu na waifurahie pumzi hiyo huku wakiwa wametulia kimya kwa muda mfupi. Ndipo amkaribishe mshiriki yeyote miongoni mwao kuomba.
Kama hatajitokeza mshiriki wa mkutano yeyote miongoni kuomba. Sala ifuatayo hapa chini yaweza kusomwa na kiongozi au mshiriki mwingine yeyote katika mkutano atakayependa kuisoma.
Mshangao Usiotegemewa. Imetolewa na Kathleen Connor, wa Pittsburgh, PA, USA

SALA

Mwenyezi Mungu muumbaji wetu. Uliyeumba mambo yote, mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo kwa namna zake mbalimbali. Wewe uliye asili ya uhai na uzima wetu tunakushukuru na kukutuza. Wewe uliye mtoa mema yote ya rohoni maishani mwetu.
Tunakuomba utuwezeshe nasi tufanye kama Bwana wetu Yesus Kristo alivyotufundisha. Utujalie kuona na kutambua vema huduma yetu uliyotuitia. Tuzione kwa wazi fulsa zote ulizoziweka kwetu na kwa majirani zetu ili tukutumikie ipasavyo kama Bwana wetu Yesu Kristo anavyopenda. Uifungue mioyo yetu na utuumbie utayari mioyoni mwetu ili tuifurahie huduma yako na kukutumikia kwa shangwe katika mazingira yanayoshangaza na kwa watu ambao hatukutegemea kuwahudumia. Kwa jina laYesu Kristo Bwana na Mwokozi wetu. Amini

Imenukuliwa kutoka kitabu cha Lifting Women's Voices, Prayers to Change the World, p. 354.

Kimenukuliwa kwa ruhusa
Hapa kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kushirikishana uzoefu mpya walioupata katika mkutano tangu walipofika jana kama:

SWALI LA TATHIMINI

Wamefahamiana na kupata muunganiko mpya na watu wengine ama marafiki wapya ambao hawakuwa wamefahamiana kabla ya mkutano huu.

Wamepata mawazo na mtazamo mpya kifikra kupitia mkutano huu.

SOMA

Utangulizi: Katika kifungu hiki cha Biblia tunakutana na habari za Hana mmoja wa wakeze 2 wa Elkana wa Nchi za Milimani katika Nchi ya Efraim. Mke mwingine wa Elkana aliyeitwa Penina alipata watoto wengi. Lakini Hana alikuwa tasa yaani mgumba, hakupata watoto. Hana alisononeka na kuumizwa sana na hali ya

kukosa watoto. Hana alitamani kupata mototo. Hivyo alimuomba sana Mungu amjalie kupata mtoto. Hana akafanya maombi ya nadhiri kwa Mungu ili apate mtoto.

Kabla ya kusoma kifungu kifuatacho cha Bibllia kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kuwa kila mmoja asikilize kwa makini neno au kifungu cha maneno yatakayomgusa sana moyoni mwake. Kisha kiongozi asome taratibu kwa sauti ya kusikika

Soma 1 Samweli 1:7-20 "Maombi ya Hana"taratibu washiriki wa mkutano wawe wameelezwa kuwa wasikilize neno au kifungu cha maneno kitakachogusa mioyo yao. Baada ya kusoma kifungu hiki cha Biblia kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kutaja neno au kifungu cha maneno kwa kutumia swali hili lifuatalo hapo chini.

KUSHIRIKISHANA
Neno gani au kifungu gani cha maneno kilchokugusa moyoni wako?
Tafadhili utushirikishe neon tu au kifungu cha maneno kwa kutaja tu usitoe maelezo kwani wakati huu si wamajadiliano

'Soma Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kuwa atamkaribisha mmoja toka miongoni mwao kusoma kwa taratibu na kwa sauti ya kusikika 1 Samwel 1: 7 – 20 kwa mara ya pili. Na kwamba inaposomwa sasa kila mmoja ajaribu kujiweka na kujiona mwenyewe ndani ya habari hii.

KUMBUKA
Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kukumbuka na kutafakari wakati ambao kila mmoja aliwahi kujisikia kama Hana. Kiongozi awape nafasi washiriki kutulia kimya kwa dakika 1.

KUSHIRIKISHANA
Baada ya washiriki wote kuwa tayari kiongozi awape nafasi kushirikisha uzoefu wao akiwakaribisha mmoja mmoja baada ya mwingine. Rejea taratibu zilizotumika katika vipindi vilivyofanyika nyuma. Kila mshiriki apewe dakika tano tu za kushirikisha na kusimulia uzoefu wake. Wakati huu wa kushirikiana kiongozi wa mkutano ndiye atakayekuwa mtunza muda Mambo yanayoshauriwa kwa washiriki wa mkutano kushirikishana na kusimuliana ni pamoja na kusimulia mambo yaliyowahi kutokea katika maisha yao, sababu zilizopelekea mambo hayo kutokea na namna walivyoweza kumuomba Mungu kuhusu mambo hayo.

Baada ya kuwa washiriki wa mkutano wameshirikishana na kusimuliana hadithi za uzoefu wao wa maisha kiongozi awape nafasi washiriki wote wa mkutano kuomba kwa sauti kubwa ya kusikika. Baada ya maombi hayo ya pamoja sala hii ifuatayo hapa chini itatumika kwa kufuga kipindi hiki cha maombi.

SALA
Na Tuombe: Mwenyezi Mungu muumbaji wetu sisi tulio uzao wa tumbo lako. Uhai na uzima tulio nao vyote vyatoka kwako. Tunakushukuru na kukutukuza kwani umetuumba na kutujalia uhai na uzima. Tunawaombea watoto wetu wote wakati huu wanaporudi majumbani kutoka mashuleni na wanaporudi mashuleni kutoka majumbani. Tunawaweka katika mikono yako kwa sababu mikono yako ndiyo yenye usalama ulio timilifu. Tunaomba kwamba uwakumbatie watoto wote na kuwalinda. Uwaepushie mabaya na hatari zote zitokazo kwa yule mwovu.
Uwabariki na kuwapa amani na furaha yako katika maisha yao.

Tunawaombea pia wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto. Roho wako Mtakatifu awaongoze na kuwajalia moyo wa upendo ili watoto wote wafikapo majumbani na mashuleni wakaribishwe kwa ukarimu na makumbatio mema ya wazazi, walezi na waangalizi wao. Tunakuomba Mungu uwape baraka zako hawa wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto ili waweze kutoa malezi mema kwa watoto kwani wao ni sehemu na washiriki pamoja nawe Mungu katika kuwapenda, kuwakuza, kuwalinda na kuwalea vema watoto wote bila kuwabagua watoto wote wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi.

Tunaomba kwamba utujalie washiriki wote wa mkutano huu moyo wa kuwapendana, kushikamana, kushirikiana na kusaidiana tukiufuata mfano wa wamama hawa waliojawa na nguvu za Roho Mtakatifu Hanna, Elizabeth na Mariam. Mama wa Samuel, Yohana na Bwana wetu Yesu Kristo. Amini.

KUKUSANYA MAWAZO NA MAONI

Sehemu hii inawaelekeza washiriki wote wa mkutano kuunganika pamoja katika kukusanya hekima na mawazo yao mithili ya uzi uwezavyo kufuma na kuunganisha pamoja. Tafadhali shirikisha washiriki wenzako wa mkutano huu juu ya uzoefu wako wa namna unavyofanya maombi kwa njia ya kujibu maswali yafuatayo:

Huwa unaomba kwa ajili ya mambo gani?

Huwa unaomba namna gani – peke yako au huwa unaomba na watu wengine?

Je huwa unaomba wakati gani?

SOMA
Utangulizi: Katika kifungu hiki cha Biblia tunakutana na habari za Hana mmoja wa wakeze 2 wa Elkana wa Nchi za Milimani katika Nchi ya Efraim. Mke mwingine wa Elkana aliyeitwa Penina alipata watoto wengi. Lakini Hana alikuwa tasa yaani mgumba, hakupata watoto. Hana alisononeka na kuumizwa sana na hali ya kukosa watoto. Hana alitamani kupata mototo. Hivyo alimuomba sana Mungu amjalie kupata mtoto. Hana akafanya maombi ya nadhiri kwa Mungu ili apate mtoto.

Kabla ya kusoma kifungu kifuatacho cha Bibllia kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kuwa kila mmoja asikilize kwa makini neno au kifungu cha maneno yatakayomgusa sana moyoni mwake. Kisha kiongozi asome taratibu kwa sauti ya kusikika

Soma 1 Samweli 1:7-20 "Maombi ya Hana"taratibu washiriki wa mkutano wawe wameelezwa kuwa wasikilize neno au kifungu cha maneno kitakachogusa mioyo yao. Baada ya kusoma kifungu hiki cha Biblia kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kutaja neno au kifungu cha maneno kwa kutumia swali hili lifuatalo hapo chini.

KUSHIRIKISHANA
Neno gani au kifungu gani cha maneno kilchokugusa moyoni wako?
Tafadhili utushirikishe neon tu au kifungu cha maneno kwa kutaja tu usitoe maelezo kwani wakati huu si wamajadiliano

'Soma Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kuwa atamkaribisha mmoja toka miongoni mwao kusoma kwa taratibu na kwa sauti ya kusikika 1 Samwel 1: 7 – 20 kwa mara ya pili. Na kwamba inaposomwa sasa kila mmoja ajaribu kujiweka na kujiona mwenyewe ndani ya habari hii.

KUMBUKA
Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kukumbuka na kutafakari wakati ambao kila mmoja aliwahi kujisikia kama Hana. Kiongozi awape nafasi washiriki kutulia kimya kwa dakika 1.

KUSHIRIKISHANA
Baada ya washiriki wote kuwa tayari kiongozi awape nafasi kushirikisha uzoefu wao akiwakaribisha mmoja mmoja baada ya mwingine. Rejea taratibu zilizotumika katika vipindi vilivyofanyika nyuma. Kila mshiriki apewe dakika tano tu za kushirikisha na kusimulia uzoefu wake. Wakati huu wa kushirikiana kiongozi wa mkutano ndiye atakayekuwa mtunza muda Mambo yanayoshauriwa kwa washiriki wa mkutano kushirikishana na kusimuliana ni pamoja na kusimulia mambo yaliyowahi kutokea katika maisha yao, sababu zilizopelekea mambo hayo kutokea na namna walivyoweza kumuomba Mungu kuhusu mambo hayo.

Baada ya kuwa washiriki wa mkutano wameshirikishana na kusimuliana hadithi za uzoefu wao wa maisha kiongozi awape nafasi washiriki wote wa mkutano kuomba kwa sauti kubwa ya kusikika. Baada ya maombi hayo ya pamoja sala hii ifuatayo hapa chini itatumika kwa kufuga kipindi hiki cha maombi.

SALA
Na Tuombe: Mwenyezi Mungu muumbaji wetu sisi tulio uzao wa tumbo lako. Uhai na uzima tulio nao vyote vyatoka kwako. Tunakushukuru na kukutukuza kwani umetuumba na kutujalia uhai na uzima. Tunawaombea watoto wetu wote wakati huu wanaporudi majumbani kutoka mashuleni na wanaporudi mashuleni kutoka majumbani. Tunawaweka katika mikono yako kwa sababu mikono yako ndiyo yenye usalama ulio timilifu. Tunaomba kwamba uwakumbatie watoto wote na kuwalinda. Uwaepushie mabaya na hatari zote zitokazo kwa yule mwovu. Uwabariki na kuwapa amani na furaha yako katika maisha yao.

Tunawaombea pia wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto. Roho wako Mtakatifu awaongoze na kuwajalia moyo wa upendo ili watoto wote wafikapo majumbani na mashuleni wakaribishwe kwa ukarimu na makumbatio mema ya wazazi, walezi na waangalizi wao. Tunakuomba Mungu uwape baraka zako hawa wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto ili waweze kutoa malezi mema kwa watoto kwani wao ni sehemu na washiriki pamoja nawe Mungu katika

kuwapenda, kuwakuza, kuwalinda na kuwalea vema watoto wote bila kuwabagua watoto wote wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi.

Tunaomba kwamba utujalie washiriki wote wa mkutano huu moyo wa kuwapendana, kushikamana, kushirikiana na kusaidiana tukiufuata mfano wa wamama hawa waliojawa na nguvu za Roho Mtakatifu Hanna, Elizabeth na Mariam. Mama wa Samuel, Yohana na Bwana wetu Yesu Kristo. Amini.

KUKUSANYA MAWAZO NA MAONI

Sehemu hii inawaelekeza washiriki wote wa mkutano kuunganika pamoja katika kukusanya hekima na mawazo yao mithili ya uzi uwezavyo kufuma na kuunganisha pamoja. Tafadhali shirikisha washiriki wenzako wa mkutano huu juu ya uzoefu wako wa namna unavyofanya maombi kwa njia ya kujibu maswali yafuatayo:

- Huwa unaomba kwa ajili ya mambo gani?
- Huwa unaomba namna gani – peke yako au huwa unaomba na watu wengine?
- Je huwa unaomba wakati gani?

Wanawake wa Kianglikana katika Maombi
Kushikamana Pamoja kwa Upendo
Maombi ya Nadhiri
Kushirikishana na kusimuliana hadithi za uzoefu wetu wa maisha ya imani
Maombi ya Hana

MKUSANYIKO
Ukaribisho
Mkutano unapoanza kiongozi awakaribishe watu wote katika mkutano kwa sauti ya kusikika vizuri.
Baada ya kuwakaribisha washiriki wa mkutano kiongozi awaombe washirik wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha kwa sauti ya kusikika asome kifungu cha Biblia kifuatacho

KIFUNGU CHA BIBLIA
Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. (Wafilipi 4:6-7).

Mshangao Usiotegemewa. Imetolewa
Na Kathleen Connor, wa Pittsburgh, PA, USA

SALA
Mwenyezi Mungu muumbaji wetu. Uliyeumba mambo yote, mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo kwa namna zake mbalimbali. Wewe uliye asili ya uhai na uzima wetu tunakushukuru na kukutuza. Wewe uliye mtoa mema yote ya rohoni maishani mwetu.
Tunakuomba utuwezeshe nasi tufanye kama Bwana wetu Yesus Kristo alivyotufundisha. Utujalie kuona na kutambua vema huduma yetu uliyotuitia. Tuzione kwa wazi fulsa zote ulizoziweka kwetu na kwa majirani zetu ili tukutumikie ipasavyo kama Bwana wetu Yesu Kristo anavyopenda.
Uifungue mioyo yetu na utuumbie utayari mioyoni mwetu ili tuifurahie huduma yako na kukutumikia kwa shangwe katika mazingira yanayoshangaza na kwa watu ambao hatukutegemea kuwahudumia. Kwa jina laYesu Kristo aliye Bwana na Mwokozi wetu.
Amini

Rejea:
Sala hii imetoholewa kutoka katika kitabu kinachoitwa

Lifting Women's Voices,
Prayers to Change the World, p. 354 Used with permission.

SWALI LA KUJITATHIMINI
Washiriki wa mkutano kushirikishana na kusimuliana hadithi zao za uzoefu tangu wamefika katika mkukutano kama wafanikiwa kufahamiana na kupata muunganiko mpya na watu ama marafiki wengine wapya ambao hawakuwa wamefahamiana kabla ya mkutano.

Kama wamepata mawazo na mtazamo mpya kifikra kupitia mkutano huu.

Utangulizi: Katika kifungu hiki cha Biblia tunakutana na habari za Hana mmoja wa wakeze 2 wa Elkana wa Nchi za Milimani katika Nchi ya Efraim. Mke mwingine wa Elkana (Penina) alipata watoto wengi. Lakini Hana alikuwa tasa yaani mgumba (hakupata watoto). Hana alisononeka na aliumizwa sana na hali ya kukosa watoto. Hana alitamani kupata mototo. Hivyo alimuomba sana Mungu amjalie kupata mtoto. Hana akafanya maombi ya nadhiri kwa Mungu ili

apate mtoto.

Kiongozi asome taratibu kwa sauti ya kusikika kifungu hiki cha Biblia

SOMA
Kadri kifungu hiki kutoka 1 Samwel 1:7-20 “Sala ya Hana” kinavyosomwa taratibu kwa sauti ya kukika kama kiongozi wa mkutano alivyoelekeza kila mmoja asikilize neno au kifungu cha maneno kinachomkugusa moyoni mwake.

1 SAMWELI 1:7-20
7 Tena mumewe akafanya hivyo mwaka kwa mwaka, hapo yule mwanamke alipokwea kwenda nyumbani kwa BWANA, ndivyo yule alivyomchokoza; basi, kwa hiyo, yeye akalia, asile chakula. 8 Elkana mumewe akamwambia, Hana, unalilia nini? Kwani huli chakula? Kwa nini moyo wako una huzuni? Je! Mimi si bora kwako kuliko watoto kumi? 9 Ndipo Hana akainuka, walipkwisha kula na kunywa huko Shilo. Naye Eli, kuhani, alikuwa akiketi kitini peke penye mwimo wa hekalu la BWANA. 10 Naye huyo mwanamke alikuwa na unchungu rohoni mwake, akamwomba BWANA akalia sana. 11 Akaweka nadhiri, akasema, Ee BWANA wa majeshi, ikiwa wewe utaliangalia teso la mjakazi wako, na kunikumbuka, wala usinisahau mimi mjakazi wako, na kunipa mimi mjakazi wako mototo mume, ndipo mimi nitakapompa BWANA huyo mototo siku zote za maisha yake, wala wembe hautamfikilia kichwani kamwe. 12 Ikawa, hapo alipodumu kuomba mbele za BWANA, Eli akamwangalia kinywa chake. 13 Basi Hana alikuwa akinena moyoni mwake; midomo yake tu ilionekana kama anena, sauti yeke isisikiwe; kwa hiyo huyo Eli alimdhania kuwa amelewa. 14 Ndipo Eli akamwambia, Je! Utakuwa mlevi hata lini? Achilia mbali divai yako. 15 Hana akajibu, akasema, Hasha! Bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye roho ya huzuni, mimi sikunywa divai wala kileo, ila nimemimina roho yangu mbele za BWANA.
16 Usimdhanie mjakazi wako kuwa ni mwanamke asiyefaa kitu; kwa kuwa katika wingi wa kuugua kwangu na kusikitika kwangu ndivyo nilivyonena hata sasa. 17 Ndipo Eli akajibu, akasema, Enenda kwa amani; na Mungu wa Israeli akujalie haja yako uliyomwomba.
18 Naye akasema, Mjakazi wako na aone kibali machoni pako. Basi huyo mwanamke akaenda zake, naye akala chakula, wala uso wake haukukunjamana tena. 19 Wakaondoka asubuhi na mapema, wakasali mbele za BWANA, kisha wakarejea na kufika nymbani kwao huko Rama; Elkana akamjua mkewe Hana; naye BWANA akamkumbuka.
20 Ikawa, wakati ulipowadia, Hana akachukua mimba na kuzaa mototo mwanamume; akamwita jina lake Samweli, akisema, Kwa kuwa nimemwomba kwa BWANA
Kiongozi
Awape nafasi washiriki wa mkutano kushirikishana na kusimuliana hadithi za uzoefu wao. Kila mmoja ataje neno tu au kufungu cha maandiko kilichomgusa moyoni mwake bila kutoa maelezo kwani wakat huu wa sasa si wa majadiliano.

KUSHIRIKISHANA
Neno gani au fungu gani la maneno yaliyokugusa moyoni wako?

Kiongozi au mmoja wa washiriki wa mkutano asome 1 Samwel 1:7-20 taratibu kwa sauti ya kusikika mara ya pili. Kadri kifungu hiki kinavyosomwa taratibu mara ya pili kila mshiriki wa mkutano ajaribu kujiweka na kujiona mwenyewe ndani ya habari hii kama kiongozi wa mkutano alivyoelekeza.
SOMA
Soma kwa sauti kubwa ya kusikika 1 Samweli 1:7-20 mara ya pili, na kadri inavyosomwa jione wewe mwenyewe ndani ya habari hii.

KUMBUKA
Kumbuka na tafakari wakati uliowhi kujisikia kama Hana.

KUSHIRIKISHANA
Kila mshiriki atajiandaa kushirikisha mkutano kwa kusimulia uzoefu wa maisha yake kwa sauti ya kusikika vizuri kwa

dakika tano tu. Atashirikisha kwa kifupi juu ya ya uzoefu wa maisha yake kama kuna wakati aliowahi kujisikia kama Hana na namna alivyomuomba Mungu.

Baada ya kushirikishana uzoefu kiongozi aombe kwa sauti ya kusika sala ifuatayo au sala nyingine yoyote itakayoongozwa na mmoja wa washiriki wa mkutano atakayejitokeza kuomba.

SALA

Na tuombe: Mwenyezi Mungu muumbaji wetu sisi tulio uzao wa tumbo lako. Uhai na uzima tulio nao vyote vyatoka kwako. Tunakushukuru na kukutukuza kwani umetuumba na kutujalia uhai na uzima. Tunawaombea watoto wetu wote wakati huu wanaporudi majumbani kutoka mashuleni na wanaporudi mashuleni kutoka majumbani. Tunawaweka katika mikono yako kwa sababu mikono yako ndiyo yenye usalama ulio timilifu. Tunaomba kwamba uwakumbatie watoto wote na kuwalinda. Uwaepushie mabaya na hatari zote zitokazo kwa yule mwovu. Uwabariki na kuwapa amani na furaha yako katika maisha yao. Tunawaombea pia wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto. Roho wako Mtakatifu awaongoze na kuwajalia moyo wa upendo ili watoto wote wafikapo majumbani na mashuleni wakaribishwe kwa ukarimu na makumbatio mema ya wazazi, walezi na waangalizi wao. Tunakuomba Mungu uwape baraka zako hawa wazazi, walezi na waangalizi wote wa watoto ili waweze kutoa malezi mema kwa watoto kwani wao ni sehemu na washiriki pamoja nawe Mungu katika kuwapenda, kuwakuza, kuwalinda na kuwalea vema watoto wote bila kuwabagua watoto wote wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi.
Tunaomba kwamba uwajalie washiriki wote wa mkutano huu moyo wa kuwapendana, kushikamana, kushirikiana. Kutunzana na kusaidiana wakiufuata mfano mzuri wa wamama hawa waliojawa na nguvu za Roho wako Mtakatifu Hanna, Elizabeth na Mariam. Mama wa Samuel, Yohana na Mama wa Bwana wetu Yesu Kristo. Amini

KUKUSANYA

Hii ni njia ya kukusanya

MAWAZO

mawazo na maoni ya washiriki wa mkutano na kuyaweka pamoja. Kila mshiriki atajibu swali na kuandika mawazo yake kisha mawazo yote yaliyoandikwa yatakusanywa na kuwekwa pamoja

Sehemu hii ya maswali imegawanyika katika sehemu 3. Tafadhali washirikishe wenzako namna unavyofanya maombi kwa kujibu maswali yafuatayo:

- Huwa unaomba kwa ajili ya mambo gani?
- Huwa unaomba namna gani – ukiwa peke yako au huwa unaomba pamoja na watu wengine?
- Huwa unaomba wakati gani?

Mwongozo wa Kiongozi
Maombi ya Shukurani
Kushirikishana na kusimuliana uzoefu wa maisha yetu ya imani
Kifungu cha Biblia Luka 1:46-55
Maombi ya Mariam – Maombi ya Shukurani

MKUSANYIKO
Kiongozi wa mkutano awakaribishe watu kadri wanavyoingia mmoja mmoja na kuketi katika viti.
Baada ya watu wote kuwa wamekaa katika viti: Kiongozi awaombe wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha asome kwa sauti ya kusikia kifungu hiki cha Biblia

KIFUNGU CHA BIBLIA
BWANA ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, Nami nimesaidiwa;
Basi, moyo wangu unashangilia,
Na kwa wimbo wangu nitamshukuru. (Zaburi 28:7)

SALA
Kiongozi awaeleze washiriki wa mkutano kwamba wataombeana wao kwa wao maombi ya mnyororo ama mzunguko kwa zamu. Kila mmoja amutamuombea mwenzake aliyeketi upande wake wa kulia. Itakapofika zamu yako utasimama na kumuombea mwenzako aliyeketi upande wa kulia kwako sala fupi kama ya sentensi moja hivi kwa sauti kubwa ya kusikika vizuri na wote.

SWALI LA KUJITATHIMINI
Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kushirikishana kwa kifupi mambo yaliyowashangaza na ambayo hawakuyategemea tangu walipofika katika mkutano huu.

Kiongozi awaeleze washiriki wa mkutano kuwa huu pia ndio wakati mzuri wa kujibu maswali yoyote yatakayoulizwa ambayo mshiriki yeyote anayo kuhusiana na shughuli za mkutano huu kwa siku hii ya leo.

SOMA
Utangulizi: Katika kifungu hiki cha Biblia tunakutana na habari za Mariamu akimsalimia binamu yake Elizabeti. Elizabeti alikuwa mjamzito wa mtazamiwa Yohana Mbatizaji, na kitoto kichanga kikaruka kwa furaha ndani ya tumbo lake mara baada ya kusikia salaamu za Mariamu. Elizabeti akajazwa nguvu za Roho Mtakatifu na kupokea uelewa wa Kimungu kwamba Mariamu amebarikiwa na mzao wa tumbo lake amebarikiwa. Elizabeti anapomsifu na kumshangilia hivi Mariamu kwa imani yake. Mariamu yeye anaitikia shangilio hili kwa mistari hii tunayokwenda kuisoma ijulikanayo kama ‘Wimbo wa Mariamu Mbarikiwa’ au ‘Magnificant’

Soma (au imba) Luka 1: 46-55 ‘Wimbo wa Mariamu Mbarikiwa’ taratibu. Wakati huu kiongozi awe ameshawakeleza ama kuwatangazia washiriki wa mkutano kusikiliza neno au fungu la maneno linalowagusa ndani ya mioyo yao.

KUSHIRIKISHANA
Neno gani au fungu gani la maneno lililowogusa ndani ya moyo yenu?

Washirikishe wenzako kwa kutaja neno tu au fungu la maneno bila maelezo kwani wakati wa sasa si wa majadiliano.

SOMA Tumia dakika 3
Kiongozi amkaribishe mmoja toka miongoni mwa washiriki wa mkutano asome Luka 1:46-55 kwa mara ya pili na kuwaeleza washiriki wa mkutano kwamba wanaposikiliza kifungu hiki kikisomwa kwao mara ya pili wajiweke wao katika nafasi ya Mariamu na kufikiria kama wao wangekuwa ndio Mariamu. Washiriki wa mkutano watatulia kimya kwa muda mfupi baada ya kifungu hiki cha Biblia kusomwa.

KUMBUKA
Kumbuka na tafakari wakati uliowahi kujisikia kama Mariamu? Washiriki wa mkutano watulie kimya kwa dakika 2

KUSHIRIKISHANA
Kila mmoja atakapokuwa tayari kiongozi awakaribishe washiriki wa mkutano kushirikishana na kusimuliana uzoefu wao. Kiongozi ndiye atakayeamua kila mmoja ashirikishe uzoefu wake kwa muda kiasi gani na ndiye atakayekuwa mtunza muda ili kila mshiriki apate nafasi ya kushirikisha uzoefu wake kwa wenzake.

Unashauriwa kushirikisha uzoefu na ushuhuda wako kwa kifupi ukihusisha mambo yafuatayo:

Kulitokea mambo gani?

Ulikuwa unafikiria nin wakati huo?

Ulikuwa ukijisikiaje wakati huo?

Baada ya hapo ulitangaza nini na ukitaka kueneza habari gani kuhusu Mungu katika ulimwengu huu tunaoishi?

KUOMBA
Kiongozi awakaribishe washiriki wote wa mkutano kuomba kwa sauti kubwa na wakati wa kufunga kipindi hiki cha maombi sala ifuatayo itumik.

Ewe Mungu wetu wa upendo utupendaye, tunakuomba utuangazie nuru yako na mwanga wako wa upendo ung’are ndani yetu mmoja mmoja kwa kadri tunavyozama ndani yako kwa uhitaji wa faraja na uongozi wa Roho wako Mtakatifu. Uwe nasi kila mmoja wetu kwa jina lake na familia yake tunapoendelea kukua ndani ya neema yako, utukuze ili tukue kwa muonekano wa wazi na zaidi ya muonekano ulio wazi. Utuwezeshe tuwe nuru ndani ya nuru, pendo ndani ya pendo na amani ndani ya amani. Amini.
Imeandikwa na Mimi A. Simson, SCHC

Wanawake wa Kiangilikana katika Maombi
Kushikamana Pamoja kwa Upendo
Maombi ya Shukurani
Kushirikishana na kusimuliana uzoefu wa maisha yetu ya imani
Kifungu cha Biblia Luka 1:46-55
Wimbo wa Mariamu

MKUSANYIKO
Ukaribisho Mkutano unapoanza kiongozi awakaribishe watu wote katika mkutano kwa furaha na sauti ya kusikika vizuri. Baada ya watu wote kuwa wamekaa katika viti: Kiongozi awaombe wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha asome kwa sauti ya kusikia kifungu hiki cha Biblia

KIFUNGU CHA BIBLIA
BWANA ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, Nami nimesaidiwa;
Basi, moyo wangu unashangilia,
Na kwa wimbo wangu nitamshukuru. (Zaburi 28:7)

SALA
Maombi ya mnyororo au mzunguko katika duara kwa zamu. Itakapofika zamu yako utasimama na kumuombea mwenzako aliyeketi upande wa kushoto kwako sala fupi kama ya sentensi moja hivi kwa sauti kubwa ya kusikika vizuri na wote.

SWWALI LA KUJITATHIMINI
Kwa kifupi washirikishe washiriki wa mkutano wenzako mambo yaliyowashangaza sana au ambayo hawakuyategemea tangu ulipofika katika mkutano huu**.**

Utangulizi: Katika kifungu hiki cha Biblia tunakutana na habari za Mariamu akimsalimia binamu yake Elizabeti. Elizabeti alikuwa mjamzito wa mtazamiwa Yohana Mbatizaji, na kitoto kichanga kikaruka kwa furaha ndani ya tumbo lake mara baada ya kusikia salaamu za Mariamu. Elizabeti akajazwa nguvu za Roho Mtakatifu na kupokea uelewa wa Kimungu kwamba Mariamu amebarikiwa na mzao wa tumbo lake amebarikiwa. Elizabeti anapomsifu na kumshangilia hivi Mariamu kwa imani yake. Mariamu yeye anaitikia shangilio hili kwa mistari hii tunayokwenda kuisoma ijulikanayo kama ‘Wimbo wa Mariamu Mbarikiwa’ au ‘Magnificant’. Kadri Luka 1: 46-55

SOMA
‘Wimbo wa Mariamu Mbarikiwa’ unaposomwa kwa sauti kubwa ya kusikika, sikiliza neno au fungu la maneno linalokugusa ndani ya moyo wako.
Wimbo wa Mariamu Mbarikiwa – New International Version (NIV)
46 Moyo wangu wamwadhimisha Bwana, 47 Na Roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu; 48 Kwa kuwa ameutazama Unyonge wa mjakazi wake. Kwa maana tazama, tokea sasa Vizazi vyote wataniita mbarikiwa; 49 Kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea makuu, Na jina lake ni takatifu. 50 Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi Kwa hao wanaomcha 51 Amefanya nguvu kwa kwa mkono wake; Amewatawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao;
52 Amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi; Na wanyonge amewakweza. 53 Wenye njaa amewashibisha mem, Na wenye mali amewaondoa mikono mitupu. 54 Amemsaidia Israeli, mtumishi wake; Ili kukumbuka rehema zake, 55 Kama alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele.

KUSHIRIKISHANA
Neno gani au fungu gani la maneno lililokugusa ndani ya moyo wako?

Taja neno tu au fungu la maneno bila maelezo kwani wakati wa sasa si wa majadiliano.

SOMA
Kiongozi asome Luka 1:46-55 kwa mara ya pili na kuwaeleza washiriki wa mkutano kwamba kila mmoja ajione na kujifikiria kama ndiye Mariamu.

KUMBUKA
Kumbuka na kutafakari wakati uliowahi kujisikia kama Mariamu!

KUSHIRIKISHANA
Kila mmoja anakaribishwa kushirikisha na kusimulia uzoefu wa maisha yake ya imani kwa kifupi. Mambo mengine yanaweza kuachwa unashauriwa kushirikisha uzoefu na ushuhuda wako kwa kifupi ukihusisha mambo yafuatayo:

Kulitokea mambo gani?

Ulikuwa unafikiria nin wakati huo?

Ulikuwa ukifikiria nini na ulikuwa ukijihisi namna gani?

Ulitangaza nini na ulitaka kisikike au ukiueneze kuhusu Mungu na kuhusu ulimwengu huu tunaoishi?

KUOMBA
Washiriki wote wa mkutano mnakaribishwa kuomba kwa sauti kubwa ya kusikika na baadaye kufunga kipindi hiki cha maombi kwa sala ifuatayo.

Ewe Mungu wetu wa upendo utupendaye, tunakuomba utuangazie nuru yako ili mwanga wako wa upendo ung'are ndani yetu mmoja mmoja kadri tunavyovunjika na kunyenyekea mbele zako. Tunaizamisha mioyo yetu na nafsi zetu ndani yako kwako kwa uhitaji wa faraja na uongozi wa Roho wako Mtakatifu. Uwe nasi katika umoja wetu tunapoendelea kukua ndani ya neema yako, ili tukuzwe vema katika muonekano ulio wazi na kuongezeka zaidi ya kukua kwa muonekano ulio wazi. Utuwezeshe tuwe nuru ndani ya nuru, pendo ndani ya pendo na amani ndani ya amani. Amini.
Imeandikwa na Mimi A. Simson, SCHC

KUKYSANYA MAONI
Kama njia ya kukusanya na kuweka mawazo na maoni yetu pamoja. Kila mmoja miongoni mwetu ataandika.

Tafadhari jibu swali lifuatalo:

Utamsimulia jinsi gani mtu mwingine namna Mungu alivyo baada ya kusikiliza na kusimuliwa uzoefu na shuhuda za watu mbalimbali za imani na kujua kwamba mungu yupo pamoja nawe.

Mwongozo wa Kiongozi
Kuambatana na kushirikiana pamoja
Kifungu cha Biblia Ruthu 1:1 -18
Ruthu na Naomi

MKUSANYIKO
Kiongozi wa mkutano awakaribishe watu kadri wanavyoingia mmoja mmoja na kuketi katika viti.

Baada ya watu wote kuwa wamekaa katika viti: Kiongozi awaombe wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha asome kwa sauti ya kusikia kifungu hiki cha Biblia

KIFUNGU CHA BIBLIA
Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. (Wafilipi 4:6-7).

Kiongozi awaeleze washiriki wa mkutano wote wavute pumzi ndefu na kisha watulie kimya kwa muda mfupi. Ndipo amkaribishe mshiriki yeyote miongoni mwao kuomba.

Kama hatajitokeza yeyote kuomba sala ifuatayo hapa chini yaweza kusomwa na kiongozi au mshiriki mwingine wa mkutano atakayependa kuisoma.

SALA
Tunakuomba Ee Bwana wa rehema utubadilishe na kutuumba upya tuwe watu wapendezwao nawe na wanaostahili kutumiwa nawe kwa mkono wako na kwa nguvu za Roho wako Mtakatifu.
Utimize mapenzi yako yote uliyo nayo ndani yetu kwa mfano wa mwana wako Yesu Kristo ili tuweze kusimama kama vyombo vya utumishi wako. Sisi ni kitu gani katika dunia hii, tunaomba utuoshe na kututakasa kwa jina la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo na utujaze hazina zako za mbinguni ili tuendelee kujitoa kwa uhiari kwa mioyo yetu kwa jina Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amina.

SOMA
Utangulizi: Kitabu cha Ruthu kinaelezea habari ya maisha mapya baina ya Ruthu na Naomi yanayovunja mipaka yao ya asili zao za mila na desturi na kuambatana pamoja. Elimeleki na mke wake Naomi na familia yao wanondoka Bethlehem kwa Moabu ili kukimbia janga la njaa. Wakiwa ugenini Ebimeleki na watoto wake wakiume wakafa na kumwacha Naomi mpweke bila msaada wa kumwezesha kuishi. Mkwewe, Ruthu Mumoabu alisisitiza kuambatana na Mama Mkwe wake yaani Naomi kwamba ataongozana naye kwenda Bethlehemu hata kama huko atakuwa mgeni.

Soma kwa sauti kubwa ya kusikika Ruthu 1:1-18

TAFAKARI
Washiriki wa mkutano wote wavute pumzi ndefu na kisha watulie kimya kwa muda mfupi huku wakiwa wamefumba macho yao.

Waza na kufikiri kama wewe ungekuwa jirani ya Naomi na Ruthu na upo nao muda Naomi anapomweleza Ruthu kurudi nymbani kwao kwa ndugu zake.

Waza, fikiri na uhisi kitu gani unchoweza kukiona juu ya uso wa Ruth anapozungumza maneno mazinto akisema “Usinisihi nikuache nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu.”

Chukua muda mfupi kutafakari kuhusu Ruthu anaacha nini na atapata nini kwa kuambatana na Naomi? (Kiongozi awapatie muda wa sekunde 25 washiriki wa mkutanao kutafakari swali hili).

Kumbuka wakati ambao uliwahi kuambatana na mtu mwingine yeyote katika shida na uhitaji wake. Katika tafakari za fikra zako kuhusu huyo mtu uliyeambatana naye vuta picha yake halisi ya wakati huo na umuone.

Shida gani iliyosababisha wewe kuambatana naye? (Kiongozi awapatie muda wa sekunde 50 washiriki wa mkutanao kutafakari swali hili).

Changamoto gani ulikutana nao katika kuambatana naye wakati wote wa shida yake? (Kiongozi awapatie muda wa sekunde 20 washiriki wa mkutanao kutafakari swali hili).

Ulipokea baraka gani kama matokeo ya kuambatana na mtu huyo? (Kiongozi awapatie muda wa sekunde 20 washiriki wa mkutanao kutafakari swali hili).

Kiongozi awaeleze washiriki wa mkutano kuanza kurejesha mawazo yao taratibu katika ukumbi wa mkutano ndipo watafumbua macho yao watakapokuwa tayari

KUSHIRIKISHA NA

Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kushirikishana mambo waliyokumbuka kuhusu wakati walipoambatana na wenzao au marafiki zao wakiwa katika shida na uhitaji. Kisha awakumbushe kuwa kila mmoja atatumia dakika tano tu kushirikisha mkutano kuhusu namna alivyoambatana na mwenzake wakati huo. Hakikisha kuwa kiongozi unatunza muda wakati wa kushirikishana. Katika kushirikishana washiriki watatakiwa kusimulia tu mazingira yaliyokuwepo na baraka walizopokea kama waambata wakati huo.

SALA

Washiriki wa mkutano waelekezwe kuambatana pamoja na kushirikiana kila mtu na mwenzake wakati wa sala ya kufunga kipindi. Kila mmoja atapata zamu ya kuomba. Wakati wa zamu yako ukifika utamuombea kwa kifupi mwenzako aliyekaa kulia kwako kwa sauti ya kusikika vizuri.

Wanawake wa Kianglikana katika Maombi
Kushikamana Pamoja kwa Upendo
Kuambatana na Kushirikiana Pamoja
Ruthu na Naomi

MKUSANYIKO
Ukaribisho Baada ya watu wote kuwa wamekaa katika viti: Kiongozi awaombe wote wakae kimya kwa muda mfupi kisha asome kwa sauti ya kusikia kifungu hiki cha Biblia

KIFUNGU CHA BIBLIA
Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. (Wafilipi 4:6-7).

SALA
Kiongozi awaombe washiriki wa mkutano wote wavute pumzi ndefu na kisha watulie kimya kwa muda mfupi. Ndipo amkaribishe mshiriki yeyote miongoni mwao kuomba.
Kama hatajitokeza yeyote kuomba sala ifuatayo hapa chini yaweza kusomwa na kiongozi au mshiriki mwingine wa mkutano atakayependa kuisoma.

Tunakuomba Ee Bwana wa rehema utubadilishe kutuumba upya tuwe watu wapendezwao nawe na wanaostahili kutumiwa nawe kwa mkono wako na kwa nguvu za Roho wako Mtakatifu.
Utimize mapenzi yako yote uliyo nayo ndani yetu kwa mfano wa mwana wako Yesu Kristo ili tuweze kusimama kama vyombo vya utumishi wako. Sisi ni kitu gani katika dunia hii, tunaomba utuoshe na kututakasa kwa jina la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo na utujaze hazina zako za mbinguni ili tuendelee kujitoa kwa uhiari kwa mioyo yetu kwa jina Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.Amina. Laura Drum, SCHC

Utangulizi: Kitabu cha Ruthu kinaelezea habari ya maisha mapya baina ya Ruthu na Naomi yanayovunja mipaka yao ya asili zao za mila na desturi na kuambatana pamoja.

Elimeleki na mke wake Naomi na familia yao wanondoka Bethlehem kwa Moabu ili kukimbia janga la njaa.

Wakiwa ugenini Ebimeleki na watoto wake wakiume wakafa na kumwacha Naomi mpweke bila msaada wa kumwezesha kuishi. Mkwewe, Ruthu Mumoabu alisisitiza kuambatana na Mama Mkwe wake yaani Naomi kwamba ataongozana naye kwenda Bethlehemu hata kama huko atakuwa mgeni.

Ruthu 1:1-18
1 Ikawa zamani za Waamuzi walipoamua, kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Bethlehemu ya Yuda., akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye na mkewe na wanawe wawili. 2 Na jina la mtu huyo aliitwa Elimeleki, na jina la mkewe Naomi, na majina ya wanawe wawili Maloni naKilioni, Waefrathi wa Bethlehemu ya Yuda. Wakafika nchi ya Moabu, wakakaa huko. 3 Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; na yule mwanamke akasalia na wanawe wawili. 4 Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la mmoja aliitwa Orpa, na jina la wa pili Ruthu. Wakakaa huko yapata miaka kumi. 5 Wakafa na Maloni na Kilioni wote wawili; na huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili, na mumewe pia. 6 Ndipo alipoondoka, yeye na wakweze, ili kurudi kutoka nchi ya Moabu; maana huko katika nchi ya Moabu amesikia ya kwamba BWANA amewajilia watu wake na kuwapa chakula. 7 Basi akatoka pale alipokuwapo, na wakweze wawili pamoja naye; wakashika njia ili kurudi mpaka nchi ya Yuda. 8 Kisha Naomi akawaambia wakweze wawili, Nendeni sasa mkarejee kila mmoja nyumbani kwa mamaye; BWANA na awatendee mema ninyi, kama ninyi mlivyowatendea mema hao waliofariki na mimi pia. 9 BWANA na awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe. Kisha akawabusu; nao wakapaza sauti zao wakalia. 10 Wakamwambia, La, sivyo;

lakini tutarudi pamoja nawe kwa watu wako. 11 Naye Naomi akasema, Enyi wanangu, mrejee; kwani kufuatana na mimi? Je! Mimi nina watoto wa kiume tena tumboni mwangu, hata wawe waume zenu? 12 Enyi wanangu, mrejee; nendeni zenu; kwa kuwa mimi ni mzee, siwezi kupata mme tena. Kama ningesema, Natumaini; kama ningepata mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kiume; 13 je! Mngesubiri hata watakapokuwa watu wazima? Mngejizuia msiwe na waume? La, sivyo, wanangu; maana ni vigumu kwangu kuliko kwenu, kwa sababu mkono wa BWANA umetoka juu yangu. 14 Nao wakapaza sauti zao, wakalia tena, na Orpa akambusu mkwewe, lakini Ruthu akaambatana naye. 15 Naye akasema, Tazama, shemeji yako amerejea kwa watu wake, na kwa mungu wake; basi urejee wewe umfuate shemeji yako. 16 Naye Ruthu akasema, Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, Na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu; 17 Pale utakapokufa nitakufa nami, Na papo hapo nitazikwa; BWANA anitende vivyo na kuzidi, ila kufa tu kutatutenga wewe nami. 18 Basi alipomwona kuwa amekaza nia yake kufuatana naye, aliacha kusema naye.

TAFAKARI
Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kuwa wavute pumzi ndefu na kisha watulie kimya kwa muda mfupi kisha awaelekeze kutafakari haya yafuatayo.

Waza na tafakari kama wewe ungekuwa jirani ya Naomi na Ruthu na upo nao muda Naomi anapomweleza Ruthu kurudi nymbani kwao kwa ndugu zake.

KUSHIRIKISHANA
Kiongozi awaelekeze washiriki wa mkutano kwamba kila mmoja ajiandae kushirikisha na kusimulia kwa dakika tatu tu habari yoyote anayoikumbuka katika maisha yake ambayo aliwahi kuambatana na mtu mwingine yeyote aliyekuea katika wakati wa shida na uhitaji. Katika kushirikisha simulizi ya uzoefu wako wa wa kuwa muambata simulia kwa kifupi tu mazingira yaliyopelekea mambo hayo kutokea na baraka za Mungu ulizopokea kwa kuambatana pamoja naye huyo mtu.

SALA
Kiongozi awaeleze washiriki wa mkutano kuwa wakati wa kufunga kipiti hiki watakuwa na maombi ya kuambatana pamoja wakiomba maombi ya mzunguko. Kila mmoja atapata zamu ya kuomba. Ukifika wakati wa zamu yako utamuombea kwa sauti kubwa ya kusikika mwenzako aliyekaa kulia kwako sala fupi ya kama sentenso moja au mbili.